# Tanzania Red Cross Society

## KANUNI ZA UCHAGUZI 2019



Mwaka huu wa 2019 ni mwaka wa uchaguzi wa viongozi kwa ngazi mbalimbali kama zilivyoainishwa katika katiba ya Tanzania Red Cross Society. Kwa mantiki hiyo, kanuni za uchaguzi zitakazotumika bila kuathiri matakwa ya katiba ni kama ifuatavyo:

1. Kamati ya Uchaguzi kama inavyofafanuliwa katika Katiba (Kifungu 40) itaratibu shughuli za uchaguzi kwa ngazi ya Taifa na Mikoa

2. Waratibu/Makatibu wa matawi ya Mikoa watahusishwa kuratibu shughuli za uchaguzi kwa ngazi za matawi madogo.

3. Nafasi za uongozi na taratibu za uchaguzi zitatangazwa kwenye matawi ili kuwafikia wanachama wote. Mtu yeyote atakayeanza kampeni mapema au kuonyesha mwenendo wa kutumia ushawishi wa fedha, basi mtu huyo hastahili kuwa miongoni mwa wagombea.

4. Ili kugombea nafasi mbalimbali, mgombea ni lazima awe Mwanachama hai na mwadilifu, awe amekwisha kuwa Mwanachama kwa muda usiopungua Mwaka mmoja kwa ngazi ya Tawi dogo isipokuwa kwa tawi jipya, Miaka miwili kwa ngazi ya Tawi la Mkoa na Miaka mitatu kwa ngazi ya Taifa.

5. Kutakuwa na gharama ya fomu kama sehemu ya kuchangia gharama za uendeshaji wa uchaguzi. Gharama za fomu kwa ngazi ya Tawi dogo ni Sh 25,000/- kwa nafasi ya Mwenyekiti na Sh 10,000/- kwa nafasi ya Mjumbe, ngazi ya Tawi la Mkoa ni Sh 300,000/- kwa nafasi ya Mwenyekiti na Sh 100,000/- kwa nafasi ya Mjumbe na ngazi ya Taifa ni Sh 1,000,000/- kwa nafasi ya Rais, Makamu wa Rais na Mweka Hazina na sh. 500,000/- kwa nafasi ya Mjumbe. Gharama za fomu kwa vijana ngazi ya Tawi dogo sh 10,000, ngazi ya Tawi la Mkoa sh 50,000 na ngazi ya Taifa ni sh 100,000/-. Pesa hizi zitawekwa kwenye akaunti maalum ya uchaguzi.

6. Fomu zikishakamilika kujazwa, wagombea wa ngazi ya Tawi la Mkoa na Tawi dogo watazi~~ta~~rudisha kwa Mratibu/Katibu wa Mkoa/Tawi dogo na wale wanaogombea ngazi ya Taifa watazirudisha ofisi ya Katibu Mkuu. Mratibu/Katibu baada ya kupokea fomu zote za wagombea ngazi ya Tawi la Mkoa, zikishapitiwa na Kamati ya Uendeshaji ya Tawi la Mkoa, ataziwasilisha ofisi ya Katibu Mkuu.

7. Kila mwanachama anayetaka kugombea ni lazima apate wadhamini (Wanachama hai) ambao ni wanachama **20** ngazi ya Taifa na kwa Rais/ Makamu wa Rais na Mweka Hazina na miongoni mwao wawe ni kutoka angalau matawi ya mikoa **8**, Wanachama **15** ngazi ya tawi la Mkoa, na Wanachama **10** ngazi ya tawi dogo.

8. Fomu zote zitarudishwa si zaidi ya saa 10:00 jioni ya tarehe ya mwisho iliyopangwa kurudishwa fomu

KANUNI ZA UCHAGUZI 2019 - TRCS

9. Mamlaka za kuchuja, kupendekeza na kupitisha majina ya wagombea kulingana na katiba ni kama ifuatavyo:

    i. NGAZI YA TAWI DOGO: Kamati ya Uendeshaji ya Tawi dogo itachuja na kupendekeza majina ya wagombea katika tawi na kuyapeleka Kamati ya Uendeshaji ya Tawi la Mkoa ambayo itapitisha majina ya wagombea watakaopigiwa kura.

    ii. NGAZI YA TAWI LA MKOA: Kamati ya Uendeshaji ya Tawi la Mkoa itachuja na kupendekeza majina ya Wagombea wa nafasi mbalimbali ngazi ya Tawil la Mkoa na kuyapeleka kwenye Kamati ya Uchaguzi ambayo itakaa pamoja na Kamati ya Mpito na kupitisha majina ya wagombea kwa ngazi ya mikoa.

    iii. NGAZI YA TAIFA: Kamati ya Uchaguzi ya Kitaifa itachuja majina ya wagombea wa nafasi mbalimbali ngazi ya Taifa kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa na kupitisha majina ya wagombea kwa ngazi ya Taifa.

    iv. Ratiba nzima ya mchakato wa uchaguzi itatolewa na Sekretariati kwa kushauriana na Kamati ya Uchaguzi.

10. Kiongozi yeyote atashika nafasi moja tu ya uongozi (Isipokuwa wale Wajumbe wa Kanda wa NEC ambao wanachaguliwa miongoni mwa Wenyeviti wa Kanda husika) kwa muda wa miaka mitano, ambapo uchaguzi mwingine utafanyika tena. Endapo mgombea atachaguliwa zaidi ya nafasi moja, itabidi ajiulzulu nafasi mojawapo.

11. Mtu yeyote anayetaka kugombea nafasi yoyote ya uongozi lazima awe na sifa zifuatazo:

    i. Awe mwanachama mwenye umri usiopungua miaka 18, isipokuwa katika klabu ya vijana
    ii. Awe mwadilifu
    iii. Awe na akili timamu
    iv. Awe amelipa ada miaka 5 mfululizo, anahudhuria vikao na shughuli za Chama, na hadaiwi na Chama
    v. Awe ni mwanachama wa kawaida (Kwa nafasi za Rais, Makamu wa Rais, Mweka hazina wa Taifa, Mwenyekiti/Makamo Mwenyekiti/Katibu wa Tawi la Mkoa na Tawi dogo ; wagombea wa nafasi hizo wasiwe viongozi wa vyama vya siasa
    vi. Kwa Klabu za Vijana; kwa nafasi za Mwenyekiti na Katibu, wagombea wa nafasi hizo wasiwe viongozi wa vyama vya siasa

12. Wagombea wa nafasi mbalimbali katika kila ngazi ni lazima wawe na elimu na sifa zifuatazo:

    i. TAWI DOGO:
        - Siyo chini ya elimu ya kidato cha nne

KANUNI ZA UCHAGUZI 2019 - TRCS

- Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Katibu, Mweka hazina, Washauri wa Maafa na Habari, Afya na Mafunzo, Mipango na maendeleo na Jinsia. Wawe na sifa na uzoefu katika uongozi

- Wajumbe wawili wawakilishi wa Tawi kwenye mkutano mkuu wa tawi la Mkoa, **Mmoja lazima awe mwanamke** (Wawe na sifa kama zilivyotajwa hapo juu).
- Mwenyekiti, Katibu na wajumbe wanne wa Baraza la vijana, pamoja na kigezo cha elimu, wawe angalau na sifa za uongozi.

ii. TAWI LA MKOA:

- Siyo chini ya elimu ya kidato cha nne na kozi zingine za utaalamu katika fani anayoomba (Professional courses)

- Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Katibu, Mweka hazina, washauri wa Maafa na habari, Afya na mafunzo, Mipango na maendeleo na Jinsia. Wawe na sifa na uzoefu katika uongozi

- Wajumbe wawili wawakilishi wa Tawi la Mkoa kwenye mkutano mkuu wa Taifa, **Mmoja lazima awe mwanamke** (Wawe na sifa kama zilivyotajwa hapo juu).

- Mwenyekiti, Katibu na wajumbe wanne wa Baraza la vijana, pamoja na kigezo cha elimu, wawe na sifa za uongozi.

iii. TAIFA:

- Siyo chini ya elimu ya Shahada ya Chuo Kikuu au elimu sawa na hiyo (equivalent education)

- Rais, Makamu wa Rais; mbali na elimu isiyo chini ya Shahada, awe na uzoefu wa uongozi katika Taasisi ya Kitaifa/Kimataifa kwa muda usiopungua miaka mitano, uwezo katika uwakilishi wa kimataifa na ushiriki katika mijadala inayohitaji upeo na uelewa wa juu wa mambo.

- Mweka hazina; elimu siyo chini ya shahada na taaluma ya Uhasibu, awe na CPA na uzoefu usiopungua miaka mitano.

- Wajumbe wa Afya na Mafunzo, Mipango na Maendeleo, Maafa na Habari na Jinsia; mbali na elimu ya shahada wawe na ujuzi, taaluma katika fani husika na uzoefu wa uongozi katika Taasisi mbalimbali usiopungua miaka mitano.

- Mwenyekiti, Katibu na wajumbe wanne wa Baraza la vijana, pamoja na kigezo cha elimu, wawe na sifa na uzoefu wa uongozi.

KANUNI ZA UCHAGUZI 2019 - TRCS

13. Mgombea atatajwa kuwa mshindi endapo atapata kura zaidi ya asilimia 50 ya kura zote zilizopigwa, isipokuwa kwa kura za makundi ambapo washindi watakuwa wale waliopata kura nyingi halali.

14. Kabla ya Uchaguzi, Kamati za Uendeshaji zitavunjwa, na Wenyeviti wanaoondoka madarakani (kama hawagombei tena) wanaweza kuchaguliwa kuwa Wenyeviti wa muda wa Mkutano wa Uchaguzi au Mwenyekiti wa muda atachaguliwa kutoka miongoni mwa wajumbe wa mkutano husika ili mradi hagombei nafasi yoyote.

15. Kwa ngazi ya Taifa, Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi ndiye atakuwa Mwenyekiti wa Mkutano Mkuu wa Uchaguzi.

16. Uchaguzi utaendeshwa kwa kura ya siri na kura zitahesabiwa na kamati iliyoteuliwa na kila mgombea atakuwa na mwakilishi wa kuangalia kura zinavyohesabiwa

17. Msimamizi wa Uchaguzi kwa ngazi husika atatangaza matokeo mara baada ya Uchaguzi.

18. Malalamiko juu ya uchaguzi yatashughulikiwa kama ilivyoanishwa katika Kifungu na. 41 cha Katiba ya TRCS.

KANUNI ZA UCHAGUZI 2019 - TRCS